JARIDA LA

# KONGAMANO LA WAANGALIZI WA HAKI ZA ARDHI VIJIJINI




## SIKU KUU YA MWANAMKE WA KIJIJINI DUNIANI



Cathbert Tomitho

### UTANGULIZI

Tarehe 14 Oktoba 2023, Taasisi ya Hakiardhi ilishirikiana na waangalizi wa haki za ardhi vijijini kuadhimisha Siku ya Mwanamke wa Kijijini duniani. Maadhimisho hayo yalifanyika Kijiji cha Msowero, Kata ya Msowero wilayani Kilosa ambapo waangalizi wapatao 122 (Me - 67, Ke - 55) walishirii pamoja na wenyeji wa pale. Mkurugenzi Mtendaji, Bw. Cathbert Tomitho, alianzisha hafla hiyo kwa kutoa hotuba ya kuwakaribisha washiriki wote, na kutoa hongera za dhati kwa waangalizi waliokuja kutoka maeneo ya mbali, kwa kujitolea gharama zao wenyewe.
Kwa heshima kubwa, Bw. Tomitho aliwaomba washiriki kusimama kwa dakika moja kumkumbuka mwangalizi wa haki za ardhi kutoka Kijiji cha Sungwa wilayani Kisarawe, Ndugu Athanas Michael, ambaye alifariki dunia mwezi Septemba 2023. Baada ya kumbukumbu hii ya kugusa mioyo, Mkurugenzi Mtendaji alimkaribisha diwani wa eneo hilo kwa ufukwenye hafla hiyo.

### UFUNGUZI

Bw. Eliudi Malekela, alifungua sherehe hiyo kwa kuanza kueleza umuhimu wa Waangalizi wa Haki za Ardhi na kutambua mchango wao katika kutatua migogoro ya ardhi katika kata hiyo. Aliongeza kwa kuwapongeza Taasisi ya Hakiardhi kwa kutoa mafunzo kwa waangalizi wa Haki za Ardhi Vijijini, mafunzo ambayo yamewajengea uwezo wa kuwasaidia wananchi kutambua haki zao za ardhi na kuzidai kwa ufanisi. Mwisho, kwa moyo mkunjufu, Diwani Malekela aliwakaribisha watu wote waliohudhuria tamasha hilo.



Eliudi A. Malekela

# MAWASILISHO YA MADA

## HAKI YA KUMILIKI NA KUDHIBITI ARDHI

Bi. Lydia William- Mwangalizi wa Haki za Ardhi kutoka kijiji cha Kimemmbe wilayani Kilindi alielezea moja kati ya changamoto zinazo wakabili wanawake wa vijijini ni haki ya umuliki na udhibiti wa ardhi. Alidokeza kuwa mara nyingi hukosa ufahamu wa haki za ardhi kuhusu umiliki wa ardhi na urithi, uwepo wa mifumo dume na mila kandamizi katika jamii.
Mifumo ya kisheria na kiutawala inaweza isilinde vya kutosha haki za wanawake, na hata kama sheria zipo, utekelezaji na ufahamu wa sheria hizi unaweza kuwa duni. "Ili kukabiliana na changamoto hii Lydia na Waangalizi wenzake wa Haki za Ardhi, walianzisha madarasa ya haki za ardhi ambapo wanakijiji hukutana mara moja kwa wiki ili kujadili masuala yanayohusiana na haki za ardhi.





## MIGOGORO YA ARDHI

Rehema Joash- Mwangalizi wa Haki za Ardhi kutoka kijiji cha Majambaa Wilaya ya Kilosa alisema "wanawake wa Vijijini wanategemea ardhi kwa ajili ya kuendesha maisha yao, kwa shughuli kama vile ukulima au ufugaji, hivyo migogoro ya ardhi inaweza kusababisha kupungua kwa uzalishaji mali, uhaba wa chakula upotevu wa mali na maisha ya watu, hali inayopelekea kushuka kwa hali ya kiuchumi.



## SHERIA NA UTOAJI HAKI

Bi. Amina Kondo Mwangalizi wa Haki za Ardhi kutoka kijiji cha Michenga Wilaya ya Kilombero aliripoti kuwa "Mifumo ya utoaji haki kama vile mabaraza ya Kata na Mahakama zimekuwa zikiwapendelea wanaume na kwaacha wanawake hivyo hupelekea wanawake kupoteza haki zao za ardhi. Mila kandamizi pia zimekuwa chachu ya ukandamizaji wa haki za wanawake.


## MUHTASARI

Tarehe 14 Oktoba 2023, Taasisi ya Hakiardhi ilishirikiana na waangalizi wa haki za ardhi vijijini katika Siku ya Mwanamke wa Kijijini duniani. Bw. Cathbert Tomitho, Mkurugenzi Mtendaji, alianzisha hafla na kutoa hongera kwa waangalizi. Diwani wa Kata ya Msowero, Bw. Eliudi Malekela, aliwapongeza waangalizi na Taasisi ya Hakiardhi kwa mafunzo yao. Mwangalizi Bi. Lydia William alielezea changamoto ya utambuzi wa haki za ardhi kwa wanawake wa vijijini. Rehema Joash alionyesha athari za migogoro ya ardhi kwa wanawake. Mwangalizi Bi. Amina Kondo alisema sheria zinapendelea wanaume. Bi. Dafrosa Daniel alieleza uporaji wa ardhi na shukrani kwa Taasisi ya Hakiardhi kwa msaada wa ushauri kisheria kupitia Waangalizi wake.


## UPORAJI ARDHI KIJIJINI MVUMI

Bi Dafrosa Daniel kutoka kijiji cha Mvumi kata ya Msowero wilayani Kilosa akieleza jinsi muwekezaji Jeet Patel alivyo pora ardhi yao. Mashamba hayo ni kati ya ardhi iliyorejeshwa na Hayati Rais John Magufuli mwaka 2017. Muwekezaji huyo aliikodisha ardhi hiyo kwa Wanavijiji kwa ada ya mwezi kiasi cha Tsh. 100,000 na mwaka kiachi cha 300,000 ambavyo haviwezi kufikiwa na wanavijiji. Licha ya kukata rufaa katika ngazi za uongozi wa serikali ya Kijiji, Dafrosa na wanawake wenzake 6 walipitia shida nyiking ikiwemo kuwekwa mahabusu na kutolewa haki ya kupata dhamana. Dafrosa anadhihirisha kuwa maafisa wa eneo hilo kwa kutolinda haki za ardhi. Anashukuru **HAKIARDHI** kwa usaidizi wa kisheria.



# MAJUMUISHO

Na Bi Subira Kibiga

Mwanachama wa Taasisi ya Hakiardhi, Bi Subira Kibiga, alitoa hotuba iliyosisimua wakati wa Kongamano la Waangalizi wa Haki za Ardhi Vijijini. Katika hotuba yake, alieleza jinsi alivyokuwa na furaha kubwa kuhusu kongamano hilo na kuwapongeza waangalizi kwa kazi yao muhimu katika harakati za kuleta mabadiliko ya ardhi.

Zaidi ya hayo, Bi Subira alitoa wito wa kutoitumia dini kama kisingizio cha vitendo vya ukatili wa kijinsia, hasa katika kutoshirikisha wanawake katika maamuzi ya familia. Alihakikisha kuwa usawa wa kijinsia na haki za wanawake ni muhimu katika jamii yetu.

Pia, alimtambua na kumpongeza Bi. Dafrosa Daniel kwa ujasiri wake katika kusimulia hadithi yake ya uporwaji wa ardhi, ambayo inawakilisha changamoto zinazo wakumba wanawake wengi Vijijini, kama ilivyotokea Kijijini Msowero.

Mwisho wa hotuba yake, Bi Subira aliwapa washiriki ladha nzuri ya shairi lililokuwa na ujumbe wa kuhamasisha mapambano kwa lengo la kuleta mabadiliko.

## MUHTASARI

Bi Subira Kibiga, mwanachama wa Taasisi ya Hakiardhi, alitoa hotuba ya kuvutia katika Kongamano la Waangalizi wa Haki za Ardhi Vijijini. Alipongeza waangalizi kwa juhudi zao katika kuleta mabadiliko ya ardhi na kutoa wito wa kutokuitumia dini kama kisingizio cha ukatili wa kijinsia.

Viongozi wa Kijiji cha Msowero na Diwani wa Kata ya Msowero walishiriki kongamano la Siku ya Mwanamke wa Kijijini na kusikiliza kero za wananchi. Walikubaliana na changamoto hizo na kuelezea changamoto wanazokutana nazo katika kutii maagizo kutoka juu. Pia, walitambua matatizo ya uporwaji wa ardhi, huku Diwani akiwa tayari kumsaidia mmoja wa waathirika.

Tamasha hilo lilihitimishwa na hotuba ya Mheshimiwa Diwani na burudani za mashairi, muziki, chakula, na vinywaji. Taasisi ya Hakiardhi iligawa machapisho kwa washiriki kwa lengo la kutoa elimu zaidi kuhusu ardhi na haki za wananchi.

## MADAI YA VIONGOZI WA SERIKALI YA KIJIJI

Viongozi wa Kijiji cha Msowero, pamoja na Diwani wa Kata ya Msowero, wilayani Kilosa, walipata fursa adhimu ya kusikiliza kero na changamoto zinazowakabili wananchi wao kupitia kongamano la kuadhimisha Siku ya Mwanamke wa Kijijini. Viongozi hao walithamini sana taarifa walizopokea kutoka kwa wananchi, kwani zilikuwa sahihi na zenye umuhimu mkubwa.

Diwani na wenyeviti wa Msowero, Mvumi, Majambaa na Madoto alizipokea changamoto hizi na waliahidi kuzifanyia kazi. Kwa pamoja waliiomba Taasisi ya Hakiardhi kwa kushirikiana na Waangalizi wa haki za ardhi kuendelea kushughulikia changamoto hizi kwa pamoja.

Hata hivyo, walifichua kwamba mara nyingine, kama viongozi wa ngazi ya chini, wanakutana na maagizo na maelekezo kutoka mamlaka za juu ambayo yanaweza kukiuka haki za wananchi wa kawaida, hivyo aliahidi kuzifikisha changamoto hizi atika vikao vya BMT kwaajiji ya utatuzi zaidi. Mwenyekiti wa Kijiji, akijitokeza mbele ya umma, alithibitisha hili. Pamoja na malalamiko ya uporwaji wa ardhi yaliyotolewa na Bi. Dafrosa, alipatakukiri kuwa hata yeye mwenyewe alikamatwa na Diwani Malekela, alikuwa tayari kuwekwa mahabusu kwa niaba ya Mwenyekiti. Hatimaye, Mh. Diwani aliahidi kulifikisha swala hilo katika vikao vya Halmashauri ya Wilaya.

Tamasha hilo lilifungwa kwa hotuba ya kuhitimisha kutoka kwa Mheshimiwa Diwani, huku watu wakipata burudani kutoka kwa mashairi, muziki, chakula, na vinywaji. Taasisi ya Hakiardhi pia ilisambaza machapisho takriban 350 ya Haki za Ardhi, Jinsia na Mabadiliko ya Tabianchi, kwa washiriki wote, kwa lengo la kutoa elimu na ufahamu zaidi kuhusu masuala ya ardhi na haki za wananchi.







